**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**
**MTIHANI WA KUHITIMU KIDATO CHA SITA**

**121/1** **KISWAHILI 1**

(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

**Muda: Saa 3** Mwaka: 2025

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **nane (8)**.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu B. Swali la **tano (5)** ni la lazima.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B ina alama **sitini (60)**.
4. Zingatia maagizo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.
5. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa **bluu** au **mweusi**.
6. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
7. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

2 502121 100013

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Soma shairi lifuatalo kwa makini kisha jibu maswali yanayofuata:

Maisha ni safari ya chombo,
Na dunia ni bahari,
Shughulika na sukani,
Mwanadamu acha kucheza na bahari.

Sisiti kusema tahadhari,
Mwanadamu twaa ngao,
Dunia humlemea mfitini,
Humsimanga mwenye choyo.

Vizuri kujiokoa, ubora kuokoana,
Kati ya maisha yetu,
Tusisahau wosia kupendana,
Tusitweze kiumbe wala mtu.

Usipaparike dunia ikikusibu,
Tafakari kwa kina, kabla hujaamua,
Dunia busara haitaki nguvu,
Maisha hayamchukizi ayachukuaye kwa heshima.

Si hekima kusema yote makosa,
Kila cheusi kina cheupe,
Si busara yote kuyapurukusha,
Katika uamuzi yafaa kuwa mpole.

**Maswali**

(a) Andika kichwa kinachofaa kwa shairi ulilosoma kwa maneno yasiyozidi mawili.

(b) Eleza kwa ufupi maana ya misemo ifuatayo kama ilivyotumika katika shairi ulilosoma.

(i) Mwanadamu twaa ngao

(ii) Dunia ni bahari

(iii) Kila cheusi kina cheupe

(c) Mwandishi katika ubeti wa tatu anawataka wanadamu waweje?

(d) Eleza kwa ufupi mawazo makuu manne ya mshairi.

(e) Mshairi anazungumzia nini katika ubeti wa mwisho?



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

2. Kwa kutumia mifano, toa hoja mbili kuonesha ubora na hoja tatu kuonesha udhaifu wa kuainisha ngeli za nomino kwa mtazamo wa kimamboleo.

3. (a) Kwa nini watumiaji wa lugha ya Kiswahili huunda maneno? Toa sababu tano.

(b) "Maneno ya lugha ya Kiswahili huundwa kwa kutumia njia mbalimbali". Thibitisha kauli hii kwa kutaja maneno mawili yaliyoundwa kwa njia zifuatazo:

(i) Mpangilio tofauti wa fonimu.

(ii) Kuunganisha maneno.

(iii) Kutohoa kutoka lugha nyingine.

(iv) Kufananisha umbo la kitu.

(v) Tanakali sauti.

4. Tafsiri sentensi zifuatazo katika lugha ya Kiingereza kwa kuzingatia tafsiri ya kisemantiki.

(i) Mwaka jana, Rais alizindua kampeni ya kudhibiti malaria.

(ii) Jana nilimtembelea mjomba wangu.

(iii) Ili ufanikiwe, ni lazima uwe na uwezo wa kufanya uamuzi.

(iv) Nilipokea taarifa kwamba baba yangu amenunua nyumba mpya.

(v) Hivyo ndivyo timu ya taifa ilivyoshindwa.

(vi) Ninawachukia watu wanaowasumbua wengine.

(vii) Asili ya lugha ya Kiswahili inavutia sana.

(viii) Tutakwenda Shule ya Sekondari Mtakuja kwa ajili ya mashindano ya mdahalo.

(ix) Tafadhali! Nipatie nakala ya Wasifu wako Binafsi.

(x) Tunakaribia kumaliza mitihani yetu.

## SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali **matatu (3)** kutoka sehemu hii. Swali la **tano (5)** ni la lazima.

5. Wewe ni mhitimu wa shahada ya Ualimu kutoka Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam. Umeona tangazo la kazi ya Ualimu wa sekondari lililotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia. Andika wasifukazi utakaoutuma kwa Katibu Mkuu wa Wizara kuomba nafasi hiyo. Jina lako liwe Sabini Tanu Ishirini.

6. Fafanua shughuli sita zilizofanywa na wakoloni nchini Tanzania zilizosaidia kukua na kuenea kwa Kiswahili.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

7. Eleza hatua tano zilizofanywa na serikali ya Waingereza katika usanifishaji wa lugha ya Kiswahili.

8. Kwa kutumia hoja sita, eleza sababu za watumiaji wa lugha kutomudu kanuni za lugha sanifu.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner